# UCHAMBUZI NA MAPENDEKEZO YA HakiElimu JUU YA VIPAUMBELE NA UPANGAJI BAJETI YA SEKTA YA ELIMU MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## Utangulizi

Mwaka wa fedha 2023/2024, ni kipindi cha tatu cha upangaji na utekelezaji wa bajeti chini ya Serikali ya Awamu ya Sita. HakiElimu tunatambua juhudi kubwa zilizofanywa na serikali hii kuboresha Sekta ya Elimu katika vipindi viwili vilivyopita. Kiwango cha Bajeti ya Sekta ya Elimu mathalani, kimeongezeka kwa wastani wa takribani asilimia 18% kutoka TZS 4,720 bilioni mwaka 2020/21, kufikia TZS 5,729 bilioni mwaka wa fedha 2022/2023.

Tunatambua kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22 TZS bilioni 353.4 fedha za mgao wa Mpango wa Mapambano dhidi ya Virusi vya UVIKO-19 zilipelekwa katika Sekta ya Elimu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 12,000 katika shule za sekondari, 3,000 katika vituo shikizi na mabweni 50 kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Serikali pia ilitoa TZS bilioni 160 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 8,000 vilivyokusudiwa kupokea ziada ya wanafunzi zaidi ya 400,000 wa kidato cha kwanza mwaka 2023.

Vile vile wigo wa utoaji 'Elimu bila Ada' umepanuliwa pia kwa kidato cha tano na cha sita. Takribani TZS billion 10.3 zinapaswa kutengwa kila mwaka kama fidia ya ada kwa wanafunzi kidato cha tano na sita. Bajeti ya "Elimu bila Ada" kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, pia imeongezeka kutoka TZS 364.2 bilioni mwaka 2021/22 hadi kufikia TZS 390 bilioni mwaka wa medha 2022/23; huku bajeti ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ikiongezeka kwa asilimia 14.7 kutoka TZS bilioni 570 mwaka 2021/2022 hadi kufikia TZS bilioni 654 mwaka 2022/2023. Fedha za kujikimu kwa mwanafunzi elimu ya juu imeongezeka pia kutoka TZS 8,500 kwa siku hadi TZS 10,000. Tunaipongeza serikali kwa uwekezaji huu kwenye Sekta ya Elimu.

Hata hivyo, mahitaji na changamoto za Sekta ya Elimu zinaongezeka kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ongozeko la wanafunzi wanodahiliwa katika ngazi zote kwa mfano udahili wa wanafunzi kidato cha kwanza umeongezeka kutoka wanafunzi 780,376 mwaka 2021 hadi wanafunzi 1,073,941 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 38 Idadi ya wanafunzi wanao faulu kidato cha sita pia imeongezeka kutoka wanafunzi 82,440 mwaka 2022 hadi kufikia 93,136 sawa na asilimia 13 huku idadi ya nafasi za udahili vyuo vikuu zikiongezeka kutoka 157,770 mwaka 2020/21 hadi 172,168 mwaka 2022/23 sawa na asilimia 9.1.

## Changamoto za Sekta ya Elimu

- **Miundombinu**

  Kwa mujibu wa Kitabu cha Takwimu za Elimu Tanzania kinachotolewa na Wizara ya Elimu na TAMISEMI (BEST) cha mwaka 2021; uwiano wa mwanafunzi kwa darasa kwa shule za msingi ni 1:74 badala ya 1:45, huku ule wa watoto wa madarasa ya awali ukiwa 1:75 badala ya 1:40 unaotakiwa. Hii inafanya shule za msingi kuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa 102,485. Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti kuu wa Hesabu za Serikali ya 2021/2022 kwa



enabling citizens to make a difference in education and democracy
Registration 00NGO/R2/000066
Board of Directors
Richard Mabala
Mwajabu Possi
Sylvester Orao
Helen Kijo-Bisimba
Illuminata Tukai
Victoria Lihiru
John Kalage

739 Mathuradas Road • P.O. Box 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Telephone: (255 22) 2151852 or 3 • Cell: (255) 754 354 681 • Fax: (255 22) 2152449 • Email: info@hakielimu.org • Website: www.hakielimu.org

Halmasauri 45 inaonyesha kuwa shule za msingi katika Halmashuri hizi zina upungufu wa madawati 158,066, matundu ya vyoo 56,530, nyumba za walimu 35,684 na upungufu wa madarasa 27,316.

- **Uhaba wa Walimu**

  Kwa mujibu wa Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2022/2023; shule za msingi nchini zinakabiliwa na uhaba wa walimu 100,958 sawa na upungufu wa asilimia 37 huku shule za sekondari zikiwa na uhaba wa walimu 74,743 sawa na asilimia 47. Pamoja na TAMISEMI kupata kibali cha kujiri walimu 13,130 kwa mwaka wa fedha 2023/24 watakaofundisha katika shule za msingi na sekondari, bado tunaona changamoto ya uhaba wa walimu itabaki kuwa walimu 162,571.

- **Ubora wa Walimu**

  Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia juu ya Viashiria vya Utoaji Huduma katika Mnyororo wa Matokeo ya Elimu (WB SDI Report, 2016); Idadi kubwa ya walimu bado hawana stadi za kitaaluma na uelimishaji zinazohitajika ili kufundisha ipasavyo. Kwa mujibu wa ripoti hii, uwezo wa maarifa miongoni mwa walimu wa Kitanzania ulikuwa duni. Ni mwalimu 1 tu kati ya walimu 5 aliyepata alama zaidi ya 80% katika jaribio lililojumuisha Kiingereza na Hesabu. Kwa ujumla ni asilimia 59 tu ya walimu walikuwa na maarifa yanayostahili. Kwa kutambua umuhimu wa mwalimu kuwa na umahiri unaoendana na wakati kitaaluma, Serikali inaweka mkazo katika Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA). Serikali imeandaa Kiunzi cha Mafunzo Endelevu Kazini kwa Walimu (Teachers' Continuous Professional Development Framework) ambacho ni nyenzo ya kuwaendeleza walimu kitaaluma na kitalaamu ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

  Changamoto kubwa katika azma na mipango hii ni kukosekana kwa bajeti toshelezi ya utoaji mafunzo stahiki kwa walimu walioko kazini. Mathalani, mwaka wa fedha 2020/21 serikali iliwezesha mafunzo kwa walimu juu ya ***utoaji wa ushauri na unasihi*** kutoka shule 174 kati 3,863 za sekondari sawa na 4.5%. Mwaka 2021/22, Serikali ilitoa mafunzo ya ***utekelezaji wa mtaala wenye kuzingatia umahiri*** kwa walimu 2,300 kati ya walimu 170,569 wa msingi sawa na 1.35% tu na walimu 1,941 tu kati ya 84,614 sawa na 2.3% wa sekondari.

- **Uendeshaji wa Shule Kupitia Ruzuku kwa Mwanafunzi**

  Serikali hutoa ruzuku kwa kwa ajili ya kugharimia uendeshaji wa shule. Fedha hizi hutumika kugharimia ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, uendeshaji wa mitihani na ukarabati. Serikali bado inatumia viwango vya ruzuku vya muda mrefu ambapo kiwanga cha TZS 10,000 kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi kwa mwaka na TZS 25,000 kwa mwanafunzi wa sekondari kwa mwaka. Hatahivyo, kutokana na mwongozo wa utoaji ruzuku serikali hupeleka TZS 6,000 kati ya Tzs 10,000 kwa mwaka kwa mwanafunzi shule za msingi na TZS 12,500 kati ya TZS 25,000 kwa mwanafunzi wa sekondari na kiasi kinachobaki

kinapelekwa wizarani kwa ajili ya ununuzi wa vitabu na vifaa vya maabara. Kiwango hiki ni kidogo na hakikidhi mahitaji ya uendeshaji wa shule.

Sambamba na ufinyu wa bajeti iko pia changamoto ya upelekaji wa ruzuku mashuleni. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Hesabu za Serikali ya Mwaka 2023, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya TZS 5.8 bilioni kati ya TZS 33.07 bilioni zilizopaswa kupelekwa katika shule za msingi na sekondari katika Halmashauri 25 zilizofanyiwa ukaguzi, hazikupelekwa kabisa. Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya CAG, kutopelekwa kwa fedha hizo kumezorotesha utoaji huduma ya elimu katika shule hizo.

- **Uthibiti Ubora**

  Katika mwaka wa fedha 2019/20, serikali ilifanya tathmini ya mazingira ya utoaji wa elimu kupitia wathibiti ubora wa nje (SQAO) katika shule za msingi 3,251 kati ya 17,804 sawa na 18.3% tu na shule za sekondari 837 kati ya 5,289 sawa na takribani 16% pekee. Mwaka 2020/21, serikali ilifanya tathmini katika shule za msingi 4,700 sawa na 26.4% na sekondari 1,200 sawa na 23% tu. Hii inaonyesha kuwa shule nyingi hazikaguliwi kwa kila mwaka na hii inatokana na ufinyu wa bajeti.

## Mapendekezo ya kuzingatia katika Upangaji wa Bajeti

- **Kuongeza Bajeti ya Sekta ya Elimu**

Kiwango ambacho serikali imekuwa ikitenga hakiwiani na viwango vilivyopendekezwa kimataifa juu ya upangaji wa bajeti ya Sekta ya Elimu. Wakati Azimio la Incheon la mwaka 2015 linazitaka nchi zilizo ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara kutenga walau asilimia 20% ya bajeti kuu za serikali zao kwa ajili ya Sekta ya Elimu; Serikali imetenga wastani wa asilimia 14% pekee kati mwaka wa fedha 2015/2016-2022/2023. Endapo serikali ingekuwa inatenga 20% ya bajeti kwenda kwenye Sekta ya Elimu, ni wazi kuwa changamoto nyingi zingeweza kutatutliwa na kuinua kiwango cha ubora wa Elimu nchini. Tunatoa rai kwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Tekinolojia, Ofisi ya Raisi TAMISEMI, na Wabunge kulitazama jambo hili na kuhakikisha bajeti ya Sekta ya Elimu inafikia asilimia 20 ya Bajeti ya Taifa.

**Jedwali la 1: Uwiano wa Bajeti ya Sekta ya Elimu na Bajeti ya Taifa**

| Bajeti (katika Tsh Bilioni) | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|---|---|
| Bajeti ya Taifa iliyopangwa | 32,476 | 33,105 | 34,879 | 37,992 | 41,481 |
| Bajeti ya Sekta ya Elimu iliyopangwa | 4,462 | 4,512 | 4,722 | 5,257 | 5,684 |
| Bajeti ya Sekta ya Elimu kama ingepangwa asilimia 20 | 6,495 | 6,621 | 6,976 | 7,598 | 8,296 |
| Upungufu wa Bajeti ya Sekta ya Elimu kwa kutopanga 20% | 2,033 | 2,109 | 2,254 | 2,341 | 2,612 |

**Chanzo:** Uchambuzi wa HakiElimu wa Vitabu vya Bajeti na Randama za Wizara ya Elimu, Sayanzi na Teknolojia

- **Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu**

Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Elimu (ESDP III) wa mwaka 2021/22-2025/26 unaainisha vipaumbele na makadirio ya bajeti inayohitajika kwenye Sekta ya Elimu. Tangu kuanza kwa utekelezaji wa ESDP III, Serikali haijaweza kutenga bajeti inayoainishwa katika Mpango huu. Mfano, wakati ESDP III ilikadiria bajeti ya TZS bilioni 7,116 kwa Mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali iliidhinisha TZS bilioni 5,645 sawa na asilimia 79.3 ya mahitaji. Kwa mwaka 2022/2023 Serikali iliidhinisha TZS 5,729 kati ya TZS bilioni 7,587 sawa na asilimia 75.5 ya pesa iliyotakiwa kutekeleza ESDP III. Mpango wa ESDP III kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umebainisha mahitaji ya bajeti ya TZS Bilioni 8,127 na hivyo basi ni rai yetu kwa Serikali na Wabunge kupanga bajeti ya Sekta ya Elimu inayoendana na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Elimu.

**Jedwali la 2: Hali ya Utekelezaji wa Mpango wa SEDP III**

| Mwaka wa Fedha | Mpango katika ESDP III (TSh. bilioni) | Bajeti halisi Sekta ya Elimu (TSh. bilioni) | Pungufu (Tsh Bilion) |
|---|---|---|---|
| 2021/22 | 7,116 | 5,260 | 1,856 |
| 2022/23 | 7,587 | 5,635 | 1,952 |
| **JUMLA KUU** | **14,703** | **10,895** | **3,808** |

**Chanzo**: Uchambuzi wa HakiElimu wa Vitabu vya Bajeti na Randama za Wizara ya Elimu 2021/2022 na 2022/2023.

- **Kuboresha Miundombinu**

Ni rai yetu kwa serikali kuja na mpango madhubuti na unaopimika wa kutatua changamoto ya miundombinu shuleni. Mapendekezo yetu ni kuwa serikali ije na mpango wa kujenga madarasa angalau 25,000 kwa mwaka (shule za msingi 20,000 na sekondari 5,000) ili kuweza kutatutua tatizo la upungufu wa madarara ndani ya miak 5. Ikiwa kila ujenzi wa darasa moja la msingi utagharimu TZS milioni 15, basi katika mwaka wa fedha 2023/24; Serikali itahitaji kutenga TZS bilioni 375 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 20,000 ya shule za msingi tu.

- **Kuboresha Viwango vya Ruzuku kwa Mwanafunzi**

Tunapendekeza viwango vya ruzuku kuongezeka hadi kufikia TZS 25,000 kwa shule za msingi kwa mwanafunzi na TZS 50,000 kwa shule za sekondari. Serikali pia ipitie upya Mwongozo wa Utoaji Ruzuku ili kuruhusu matumizi ya fedha ya ruzuku katika kutoa huduma ya chakula shuleni pamoja na ununuzi wa SODO kwa watoto wa kike wanaohitaji kujihifadhi nyakati za hedhi. Ikumbukwe pia kuwa Serikali imeandaa Mwongozo wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe Shuleni. Mwongozo huo unaelekeza utolewaji wa huduma ya chakula shuleni katika viwango stahiki ili kuboresha afya na mahudhurio ya wanafunzi. Ni muhimu kwa Serikali wazazi pamoja na wadau wengine kuzingatia Mwongozo huu wakati wa upangaji wa bajeti ili kuziwezesha shule kugharamia lishe shuleni.

- **Kuweka Mpango wa Kuajiri Walimu**

Mwaka wa fedha 2021/22, HakiElimu tulishauri serikali kuweka mpango wa muda mrefu (Miaka 5) wa kumaliza tatizo la uhaba wa walimu nchini. Katika mapendekezo yetu tuliishauri Serikali kuweka mkakati wa kupanga bajeti ya kuajiri walimu angalau 40,000 kwa mwaka (Msingi 25,000 na Sekondari

15,000). Mpango huu utapelekea kumaliza kabisa tatizo la uhaba wa walimu wa shule za msingi na sekondari kwa miaka mitano ijayo. Ni mapendekezo yetu kuwa serikali iongeze idadi ya walimu wanaojajiriwa hadi kufikia 40,000 kwa mwaka wa fedha 2023/24.

- **Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo na Mitaala**

Tunafahamu kuwa Serikali imeendelea na mchakato wa kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo pamoja na Mitaala tangu mwaka 2021/2022. Miaka miwili imeshapita na bado mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo hayajakamilika. HakiElimu tunatoa rai kwa serikali kuongeza jitihada ili kukamilisha mapitio ya Sera na Mitaala katika mwaka wa fedha 2023/2024 ili tuweze kupata Sera na Mitaala iliyo bora na inayokidhi mahitaji ya Karne ya 21 na maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla.

## Tunapata Wapi Fedha ili Kuongeza Bajeti ya Sekta ya Elimu

Ripoti za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zinaonesha iko mianya mingi ya matumizi mabaya ya fedha za umma na udhaifu mkubwa katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kama changamoto na udhaifu huu ungeshughulikiwa ipasavyo fedha nyingi zingeweza kuokolewa na kuelekezwa katika maendeleo ya Taifa ikiwemo utatuzi wa changamoto kwenye Sekta ya Elimu.

Mathalani, kwa mujibu wa taarifa ya CAG mwaka wa fedha 2021/22; TZS bilioni 88.42 zilizotolewa kama mikopo kwa makundi ya Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) 180 nchini, hazikurejeshwa. Mamlaka 98 hazikuwasilisha kiasi cha TZS bilioni 15.19 zilizokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato na TZS bilioni 8.99 zilikopeshwa na Halmashauri lakini hazikurejeshwa. Ripoti hiyo inaonesha pia Mamlaka za Serikali za Mtaa kushindwa kukusanya TZS 76.56 bilioni walizotakiwa kukusanya kutokana na mapato ya vizimba, tozo, ushuru na leseni kama ilivyotarajiwa.

Aidha Ripoti inaonesha ubadhirifu katika baadhi ya miradi mikubwa. Mfano, Shirika la Reli nchini (TRC) lilisababisha hasara ya TZS Bilioni 503.2 kwa kumkataa mzabuni aliyetaka kulipwa Sh bilioni 616.4 na kumpa kazi mzabuni wa Sh trilioni 1.119 sawa na ongezeko la asilimia 82 isiyokuwa na ulazima. TSZ 632 milioni za Mradi wa EP4R zilipotea katika ujenzi wa chuo kipya cha uwalimu Sumbawanga chenye kugharimu bilioni 3. Ripoti pia inaonesha zaidi ya TZS bilioni 50 zilitumika kununua vifaa tiba hewa katika sekta ya afya.

Taarifa inabainisha pia ubadhilifu katika Wizara ya Ujenzi ambayo haikukusanya TZS bilioni 41.4 iliyotakiwa kutozwa wakati wa kusafirisha mizigo mizito, huku wakala wa Majengo (TBA) na Mahakama pia hazikutoza TZS 8.43 billioni wakati wa kutoa huduma kama zinavyopaswa. Ripoti inasema pia, Taasisi za Serikali kuu zilitumia TZS bilioni 3.39 huku Mamlaka za Serikali za Mitaa zikitumia TZS bilioni 26.28 kununua mangari hewa.

Maeneo haya machache ya Taarifa ya CAG 2021/22 yanaonesha serikali imepoteza zaidi ya TZS **813.5 billioni**. Ikiwa Serikali kwa kutumia **TZS bilioni 353.4** fedha za mgao wa mapambano dhidi ya

UVIKO-19 iliwezesha ujenzi wa madarasa 12,000 katika shule za sekondari, 3,000 katika vituo shikizi na mabweni 50 kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu; TZS **813.5 billioni** zingeweza kujenga miundo mbinu ya sekta ya elimu zaidi ya mara mbili ya miundo mbinu iliyojengwa kwa fedha za UVIKO 19.

Ni matumaini yetu kuwa ushauri mapendekezo haya yatazingatiwa katika upngaji wa bajeti ya Sekta ya Elimu katika mwaka huu wa fedha.

Ahsanteni,

**Dkt. John Kalage**
Mkurugenzi Mtendaji